# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU
# SHULE YA SEKONDARI NANDEMBO

Namba za simu

Mkuu wa shule: 0768627325/ 0627427325

Makamu Mkuu wa Shule: 0756899591/0788944588

Matron/Patron: 0783232760/0753018187

Email: nandembosecondaryschool@gmail.com

Blog: nandembosec.wordpress.com

Shule ya Sekondari Nandembo,

S.L.P 238,

**TUNDURU.**

Tarehe 20/04/2024.

---

Kumb. Na. NSS/U.KIDT.V/V.I/14

**Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi**
…………………………............
S.L.P ……………………….……..
………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANDEMBO HALMASHAURI YA WILAYA TUNDURU, MKOA WA RUVUMA MWAKA 2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024 na atasoma Tahasusi ya ………. Shule ya Sekondari Nandembo ipo umbali wa Kilometa 18 Kaskazini Magharibi mwa mji wa Tunduru katika barabara kuu inayoelekea Songea. Usafiri wa basi kutoka Tunduru mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Tunduru. Nauli ya mabasi yanayoelekea Songea ni shilingi 1,000/= Nauli ya Bajaji kutoka Tunduru mjini hadi Nandembo stendi shilingi 2,000/=. Nauli ya Bodaboda/pikipiki kutoka Nandembo stendi hadi shuleni shilingi 1,000/=. Aidha gharama za kukodi Bajaji kutoka Tunduru mjini hadi Shuleni ni kati ya Tshs 8,000/= hadi 10,000/=

   Muhula wa masomo wa mwaka **2024/2025** unaanza tarehe **……./……/2024**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…../…../2024. MWISHO** wa kuripoti shuleni ni tarehe **…../…../2024.**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

   **2.1 Sare ya Shule**

   a) Sare ya shule hii ni: Sketi mbili (2) rangi ya 'light blue' mshono wa Linda Box, ndefu ikaribie kisigino.
   b) Mashati meupe mawili (2) mikono mirefu.
   c) Rangi ya hijab (kijuba) ifanane na sare ya shule, ifunike kifua cha mwanafunzi. Pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
   d) Sare ya michezo kwa shule hii ni: Track suit rangi ya blue bahari jozi moja na Tshirt nyekundu isiyo na maandishi zitavaliwa wakati wa michezo.
   e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
   f) Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
   g) Sweta moja rangi ya '**light blue'** (rangi ya sketi)
   h) Nguo za kushindia (shamba dress): Magauni mawili (2) **rangi ya 'dark blue' mshono wa solo** iwe ndefu usawa wa kisigino.

NANDEMBO HIGH SCHO

i) Skafu moja (1) rangi ya 'light blue' (rangi ya sketi)
j) Tshirt yenye nembo ya shule Tshs. **13,000/=** ilipwe/iletwe shuleni

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**-

i. Karatasi **Bunda moja (Ream) A4** kila Muhula (**Bunda mbili (2)** kwa mwaka).
ii. Aje na kadi ya **Bima ya Afya** (NHIF) na kama hana aje na fedha ya matibabu.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iv. Godoro moja 1) futi $2\frac{1}{2}$ x 6"
v. Mashuka mawili (2) rangi ya pink, blanketi 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe)
vii. Ndoo mbili ndogo (lita kumi) zenye mifuniko
viii. Jembe 1, reki 1, kwanja 1, mopa 1, mfagio laini wa ndani 1 na mgumu 1 (brush)
ix. Dawa ya chooni lita 1 (toilet deodorant)
x. Dissecting Kit kwa wanafunzi wa Bioloji.
xi. Koti la Maabara jeupe (Wanaosoma sayansi)
xii. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi
xiii. Madaftari (counter book) - 10 na vifaa vya kuandikia

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3 | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **80,000.00** |

**NB:** **MICHANGO YA SHULE** ilipwe kwenye Akaunti ya Shule **A/C No.70901100067** katika Benki ya **NMB - Nandembo Secondary School.** Na mwanafunzi afike na Hati ya Malipo ya Benki (BPS). **Fedha Taslimu Hazitapokelewa Shuleni.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria Na. 10** ya mwaka **1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoljia, yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule.**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

NANDEMBO HIGH SCHOOL

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi **haruhusiwi kubadili dini** wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NANDEMBO HIGH SCHOOL

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu:**
    a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali;
    b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai;
    c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule; na
    d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Moto wa Shule**

# "ELIMU KWA MAFANIKIO"

Nakutakia maandalizi mema, KARIBU SANA NANDEMBO SEKONDARI

**Ndunguru G.K**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
NANDEMBO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 238 TUNDURU

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule: **0768627325/ 0627427325**
- Makamu Mkuu wa Shule**: 0756899591/0788944588**
- Mwandamizi Taaluma**: 0678533914/0625858404**
- Mwandamizi Malezi**: 0715617123**

NANDEMBO HIGH SCHOOL

*Kiambatanisho 1.*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

RUVUMA

0687201313

Nandembo secondary School,

P. O. BOX 238,

TUNDURU.

Date…………………………

THE MEDICAL OFFICER,
……………………………….
………………………………
……………………………..

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a medical officer

1. Full name: ……………………………………………………………………………………
2. Age: ………………………………………… (Years). Sex: …………………………
3. Blood counts (red and white) ………………………………………………………
4. Stood Examination ……………………………………………………………………
5. Urinalysis …………………………………………………………………………
6. Syphilis test ………………………………………………………………………………
7. Venereal disease test ……………………………………………………………
8. TB test ………………………………………………………………………………
9. Eye test ………………………………………………………………………………
10. Ear test ………………………………………………………………………………
11. Chest …………………………………………………………………………………
12. Spleen ………………………………………………………………………………
13. Abdomen ……………………………………………………………………………
14. Test for Pregnancy ……………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION (if any) e.g. Physical defects or impairment(s) arm, leg, infections chronic or family disease etc.

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named student is fit/unfit to pursue education as stated above.

Signature…………………

Designation …………………

Station …………………………

Date…………………………………

NANDEMBO HIGH SCHOOL

*Kiambatanisho 2.*

## SHULE YA SEKONDARI NANDEMBO

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

**(A) TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi (kama lilivyotumika kwenye cheti cha kidato cha nne)…………………………………………………………………………………….
2. Mahali ulipozaliwa: Mtaa/kijiji: …………………… Kata: ……………………… Tarafa: …………………… Wilaya: …………………… Mkoa: …………………… Dini…………………… Kabila………………………………….
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………….
4. Shule uliyohitimu Darasa la saba…………………………………………………
5. Shule uliyohitimu kidato cha nne…………………………… Ipo Wilaya ya: ……………………… Mkoa wa: ……………………………….
6. Kidato unachokuja kujiunga hapa shuleni ………………………………………..

**AHADI YA MWANAFUNZI**

1. Mimi ……………………………………………………………………………………… ninakubali kujiunga kidato cha………………… tahasusi ………… katika shule ya sekondari ya Nandembo.

2. Ninaahidi kwamba nitakuwa mwanafunzi bora mwenye bidii na utii kwa sheria za shule, walimu, walezi na viongozi wa shule kwa muda wote nitakapokuwepo shuleni.
3. Pia ninaahidi kutoshiriki katika migomo yoyote, kufanya fujo au makosa yoyote ya jinai kwa kipindi chote nitakachokuwa shuleni.
4. Ninaahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii katika masomo muda wote.
   Tarehe: ………………………………. Saini: ……………………………………..

**(B) TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina la baba ………………………………………………………… Hai/amekufa
2. Jina la mama ……………………………………………………… Hai/ amekufa
3. Jina kamili la mlezi (kama huna mzazi) ………………………………………….
4. Uhusiano na mlezi …………………………………………………………………
5. Kazi ya mzazi/mlezi ………………………………………………………………
6. Dini……………………………………………………………………………………
7. Kama ni mkulima zao la muhimu analotegemea ni ……………………………
8. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni ………………………………………………
9. Mahali anapoishi mzazi/mlezi
   (a) Kijiji/Mtaa: ........................................................................................
   (b) Kata: ..................................................................................................
   (c) Tarafa: ...............................................................................................
   (d) Anuani ya mzazi/mlezi: ......................................................................
   ..............................................................................................................
   (e) Namba ya simu: ..................................................................................
   (f) Email: .................................................................................................

NANDEMBO HIGH SCHOOL

## NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

**JINA LA MWANAFUNZI..........................................................................**

**KIDATO CHA.................................. TAHASUSI YA.......................................**

Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao hii itasaidia kutoa taarifa endapo tatizo litatokea. Hatutaki majina ya Ndugu bandia. Tunaomba mzingatie hilo kwa ajili ya usalama wa mtoto wako. Kama una ndugu karibu na mazingira ya shule, tafadhali tunaomba umtambulishe kwa kujaza taarifa zake katika fomu hii.

1. (a) Jina: ...........................................................

   (b) Uhusiano: ...................................................

   (c) Anuani: .......................................................

   (d) Namba ya simu: ...........................................

   Bandika picha yake hapa

2. (a) Jina: ...........................................................

   (b) Uhusiano: ...................................................

   (c) Anuani: .......................................................

   (d) Namba ya simu: ...........................................

   Bandika picha yake hapa

3. (a) Jina: ...........................................................

   (b) Uhusiano: ...................................................

   (c) Anuani: .......................................................

   (d) Namba ya simu: ...........................................

   Bandika picha yake hapa

4. (a) Jina: ...........................................................

   (b) Uhusiano: ...................................................

   (c) Anuani: .......................................................

   (d) Namba ya simu: ...........................................

   Bandika picha yake hapa

Sahihi ya Mzazi/Mlezi...................................................

Tarehe...................................................

NANDEMBO HIGH SCHOOL

*Kiambatanisho 3*

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.**

1. Mimi………………………………………………………ninakubali/sikubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari Nandembo kuanzia tarehe. ………………………………
2. Ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua/fomu ya maelekezo/maagizo ya kujiunga na shule (Joining Instruction).
3. Nitahakikisha kwamba mtoto wangu amesoma sheria zote muhimu za shule na kuzielewa.
4. Ninaahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii katika masomo.
5. Ninaahidi kuwa mtoto wangu hatajihusisha na migomo, fujo au vitendo vya uvunjifu wa amani awapo shuleni.
6. Awapo shuleni mtoto wangu alelewe katika maadili ya dini ya ………………
7. Anuani yangu ya kudumu ni:
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
8. Namba ya simu: ……………………………………………………………………………
9. Andika namba ya simu iliyounganishwa na **WHATSAPP** kama ipo ili uweze kuunganishwa kwenye kundi la walimu na wazazi kwa ajili ya kutumiwa Taarifa za maendeleo ya kitaaluma ikiwemo matokeo ya kila mtihani atakaofanya mwanao awapo shuleni.

   ……………………………………………………………………………………………

**SAINI: ……………………………………**

**TAREHE: ………………………………**

NANDEMBO HIGH SCHOOL

*Kiambatanisho 4*

# SHULE YA SEKONDARI NANDEMBO

## ORODHA YA VITABU

Orodha ya vitabu vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Mzazi/Mlezi unaweza kumununulia mwanao baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo katika **Tahasusi** aliyopangiwa yaani HGL (History, Geography na English Language) au HKL (History, Kiswahili na English Language) au CBG (Chemistry, Biology na Geography) General studies ni kwa wote.

**A. HISTORY**

1. TIE (2016) History for Secondary Schools: Form Five - Tanzania Institute of Education.
2. TIE (2016) History for Secondary Schools Form Six, Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education
3. Tumaini, S.C.K (2010) Contemporary Historical Events: Advanced Level History one, Dar es Salaam: Shgibitali & Sons publishers
4. Yassin S. (..) Essentials in Advanced Levels History Paper 2, Dar es Salaam

**B. ENGLISH LANGUAGE**

1. Asheri, N. (2014) Advanced Level English: A Practical Approach,3rd Ed., Dar es Salaam: Good Books Publishers
2. John, J. (2012) Advanced English Language: Form 5 & 6, Dar es Salaam: Oxford University Press.
3. Advanced Learners Dictionary - Oxford

**POETRY**

(a) Selected Poems. - Tanzania Institute of Education
(b) The wonderful Surgeon and Other Poems. – Charles Mloka - Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

**NOVELS AND SHORT STORIES (walau vitabu viwili)**

(a) The Beautyful Ones Are Not Yet Born - Ayi Kwei Armah
(b) A Man of the People - Chinua Achebe
(c) Divine Providence - Severin N. Ndunguru
(d) His Excellence Head of State - Danny Safo
(e) A season OF Waiting – David Omowale
(f) Vanishing Shadows - Namige Kayondo

**PLAYS (walau vitabu viwili)**

(a) Betrayal in the City - Francis Imbunga
(b) I Will Marry When I Want - Ngugi wa Thiong’o and Ngugi wa Mirii
(c) Lwanda Magere - Okoiti Omtatah
(d) An Enemy of the People - Henrik Ibsen
(e) Black Mamba - John Ruganda

NANDEMBO HIGH SCHOOL

**C. GEOGRAPHY**

1. Geography for Secondary Schools: Form Five. - Tanzania Institute of Education (2016)
2. Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying. – Zisti Kamili
3. Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges. – Ahmed Lubwama
4. A Comprehensive Approach to Physical Geography – D.T. Msabila

**D. KISWAHILI**

**(i) KISWAHILI 1**

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010)
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI

**(ii) FASIHI**

1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford university Press
2. Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwine na Masebo

**TAMTHILIA** (**walau vitabu viwili**)

1) Kivuli Kinaish – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
2) Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3) Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4) Morani –Emanuel Mbogo (1993)

**RIWAYA** (**walau vitabu viwili**)

1) Vuta ni Kuvute, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)
2) Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
3) Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4) Usiku Utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

**USHAIRI** (**walau vitabu viwili**)

1) Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed.) – Haji Gora Haji (1995) - TUKI
2) Chungu Tamu – Theobald Mvungi
3) Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers
4) Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

**E. GENERAL STUDIES**

1. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6.
2. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary Schools,

NANDEMBO HIGH SCHOOL

### F. CHEMISTRY

1. Advanced level Physical Chemistry with General Chemistry (Ape Network)
2. Physical Chemistry with General Chemistry – Mark Daniel and Hermes Damians
3. Chemistry for Secondary Schools, Form six (TIE) – Prof. Eustella P. Bhalalusesa
4. Conceptual Chemistry, Class XI & XII (By S.Chand)
5. A-Level Chemistry 4$^{th}$ Edition. – E.N. Ramsden

### G. BIOLOGY

1. Advanced Biology 1: Review 4$^{th}$ Ed. – Cyrus Vendelin and Mark Daniel
2. Guidance to Dissection by H.G.QROWETT
3. Biological Science 3$^{rd}$ Ed. – D.J.Taylor, N.P.O. Green and G.W. Stout
4. New Understanding Biology For Advanced Level 4$^{th}$ Ed. – Oxford University Press

### H. BASIC APPLIED MATHEMATICS (kwa wanaosoma sayansi)

1. Basic Applied Mathematics Review 2$^{nd}$ Ed. – Immaculate Mosha and Yahya Kawa
2. Basic Applied for Secondary School Form Five – TIE
3. Basic Applied for Secondary School Form Six – TIE

NANDEMBO HIGH SCHOOL

*Kiambatanisho 5.*

(a) **Mwonekano katika Sare za shule**



**Mwonekano wa skafu kwa nyuma**



**Shamba Dress**

